**MTIHANI WA PAMOJA WA SUKELLEMO 2022**

**102/ 2 KISWAHILI Karatasi ya Pili**

**LUGHA**

**Muda: Saa 2 ½**

**Jina…………………………………………Nambari ya Mtahiniwa……………………**

**Sahihi ya Mtahiniwa…………………Kidato………….. Tarehe…………….………..**

**Maagizo**

*a) Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

*b) Weka sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoaciwa hapo juu.*

*c) Jibu maswali yote*

*d) Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu cha maswali.*

*e) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

*f) Karatasi hii ina kurasa 10 zilizopigwa chapa.*

**g) Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

**Kwa Matumizi Ya Mtahini Pekee:**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| Jumla | 80 | |

visit www.freekcsepastpapers.com for more revision content

**1. UFAHAMU.(alama 15)**

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Ulikuwa usiku wa manane, mavia hatawahi kuyasau yaliyotokea usiku huo na madhara yaliyoikumba aila yake; ambayo hadi wa leo huwasumbua na kuwafuata kila waendako na hata kuishi. Matokeo ya kitendo kilichotekelezwa na nduguye Mnuna yamesalia kama dondandugu moyoni mwake. Yeye hujaribu kuyafutilia mbali lakini yanakataa katakata kuondoka fuvuni mwake hasa anapomtazama nduguyue mdogo. Maria alikuwa akidurusu somo la Fizikia. Abdalla kakake mkubwa akimpa Tom wosia. "Tom, itakuwa bora ikiwa mtanena kwa amani na baba kuhusu tofauti zenu."

Hamna haja ya kumrushia cheche za matusi, kumbuka kuwa heshima kwa mzazi ni taadhima kwa mterehemezi matokeo yake ni baraka na sudi tele." Tom alikinai kuyatilia maanani mawaidha ya kaka yake. Akajitia hamnazo na kudai kuwa baba yake amemdunisha kwa muda mrefu na angemfunza adabu. Watu wote katika familia walijaribu kumsihi lakini ikawa bure.

"Upyaro haufai ndugu yangu. Hata kama una kimo kikubwa kuliko baba kumbuka kuwa ndiye mzazi aliyekulea wewe." Alidokeza Maria.

Baba yake Maria, Mugambi, alikuwa amechoshwa na vitendo vya mwanawe vya kutumia dawa za kulevya. Aghalabu Tom alikuwa akizua rabsha kila jioni baada ya kutoka shule. Mugambi alikuwa amemwadhibu mwanawe na hata kumshtaki katika kituo cha polisi lakini hakubadilika. Watu walisema kuwa alikuwa na fedha nyingi kutokana na ulanguzi wa mihadarati. Jambo hili humwezesha kuhepa mitego ya askari kwa kuzunguka mbuyu. Tom akawa asiyesikia la mwadhini wala mteka maji msikitini.

"Mzee ninataka unipe urithi wangu, la sivyo leo utaiona dunia hii paa!" Tom akamtisha baba yake. Mugambi akaja juu na kumwambia mwanawe kuwa umri wake haukutosha kupewa urithi. Ingembidi akamilishe masomo kwanza ajijengee msingi bora wa maisha yake ya kesho na hata kupata mali yake mwenyewe." Mimi si mtoto. Ninataka uelewe kuwa leo ikiwa siku yangu ya mwisho kuhudhuria shule. Hiyo elimu ya wakoloni imenichosha! Katu sisomi tena." akasema Tom. Punde si punde Mugambi alipandwa na za mkizi na kumwandama mwanawe kwa makonde ikawa vurugu si vurugu. Kuwamamanua bila mafanikio. Licha ya kuumizwa na kujeruhiwa sehemu kadha za mwili wake, Tom alishikilia kikiki na kuendelea kupambana na baba yake. Mama yake alipoona maji yamezidi unga, aliamua kuingilia kati na liwe liwalo kwa bahati mbaya Tom alimrushia teke la ubavuni wake na kumwangusha chini pu!

"Aghrr! Haya yote unayotufanyia sisi wazazi wako yatakufuata daima." Mugambi alilaani huku akigaragara sakafuni kwa maumivu tele. "Ninataka uniuwe leo, siwezi kukulea mwa dhiki na taabu tele halafu unikosee mimi na mamako heshima namna hii utaona kilichomtoa kanga manyoya," Mugambi alimwambia mwanawe akiwa na uchungu mwingi moyoni. Majirani mimi nikiwemo walikuja kujionea sinema ya bure: "Teresia, unaona namna Tom alivyowakosea wazazi wangu heshima?" Maria aliniuliza kwa muda mrefu familia yetu imekosa amani kwa sababu ya Tom kuzua fujo mara kwa mara. Amewajeruhi wazazi wangu mara nyingi huku akivivunjavunja kenyekenye vyombo vya mama. Tandabelua anaozua Tom hunifanya mimi na ndugu zangu kutohudhuria shule wakati mwingine. Huwa tunahofia kuangamizwa kwa wazazi wetu, hivyo kubaki nyumbani kama walinzi wao. Tom amegeuka hayawani. Hajali habali." alinieleza Maria huku machozi yakimtiririka tiriri, njia mbili mbili.

Nyumba yetu ilikuwa mita chache kutoka nyumbani kwa akina Maria. Nilikuwa wa kwanza kushuhudia Tom akiwatendea wazazi wake unyama pamoja na ndugu yake Abdallah. Alikuwa amewajeruhi vibaya. Abdallah

visit www.freekcsepastpapers.com for more revision content

www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com

alipojaribu kuwasaidia wavyele wake alirushiwa upanga uliompata barabara kwenye kisigino. Ninakumbuka namna Abdallah alivyochechemea kwa uchungu mwingi huku akiwa ameyauma meno. Ninakumbuka vyema. Kama wote walioshuhudia unyama wa Tom walilengwalengwa na machozi huku wakiulaani. Wanakijiji cha umoja waliamua kumpiga kitutu na kumfukuza. Alipotambua wamemzidi nguvu, alikimbia kiswara na kuelekea upande wa chini. Kwa bahati mbaya, alianguka shimoni na kuvunjika miguu yote miwili. Aketipo na kudhukuru vitendo alivyokuwa akiifanyia familia yake Tom hupatwa na majuto makubwa. Leo ameamini kuwa majuto ni mjukuu.

**Maswali**.

(a) Eleza msimamo wa Mugambi kuhusu kumpa mwanawe urithi. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

……………………………

(b) Taja sababu kuu iliyomfanya Tom kutekeleza vitendo vya kinyama. (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………..

(c) Kwa kurejelea kifungu, thibitisha jinsi uozo ulivyokithiri katika jamii ya umoja. (alama 4)

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

……………………………

(d) Fafanua wasifu wa Tom kulingana na taarifa hii. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………

(e) Eleza suala la uwajibikaji kama linavyojitokeza katika taarifa. (alama 3)

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………

(f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika taarifa. (alama 3)

(i) sudi ……………………………………………………………………………………………..

visit www.freekcsepastpapers.com for more revision content

www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com

www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com

(ii) kuzunguka mbuyu

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

(iii) kuwamamanua

……………………………………………………………………………………………………

**2. UFUPISHO**

Soma kifungu kifuatacho cha habari kisha ujibu maswali yanayofuatia

Utoaji wa Huduma ya Kwanza

Inaaminika kuwa majeruhi wengi katika mikasa ya ajali huaga au huathirika vibaya Zaidi kutokana na hali mbaya mbaya ya uokoaji. Watu wengi ambao hujitolea kuokoa majeruhi baada ya ajali kama za barabarani, maporomoko ya ardhi au nyumba huwa hawang'amui hata chembe jinsi ya kukabiliana na uokoaji. Hatima ya juhudi zao ambazo hulenga kutenga mema ni kuathirika Zaidi kwa majeruhi.

visit www.freekcsepastpapers.com for more revision content

Hali ya uokoaji inaweza kurekebishwa kwa kutoa elimu ya huduma ya kwanza kwa umma. Elimu hii yahitajika na kila mkenya kwani mikasa ya ajali ya barabarani na nyinginezo inaendelea kutokea kila siku. Ajali zinapotokea, si ajabu kuona makundi ya waokoaji yakibeba majeruhi hobelahobela bila kuzingatia madhara yanayoweza kuwaongezea kutokana na ubebaji wao. Kutojua namna ya kumbeba majeruhi kunaweza kumhatarisha nahata kusababisha kifo.

Kuna mambo mbalimbali ambayo makundi ya waokoaji yanatakiwa kuzingatia wakati wa huduma ya kuokoa. Kwanza ni muhimu kuchunguza kama kuna hatari yoyote inayoweza kutokea na kuwatia majeruhi na waokoaji hatarini Zaidi. Makundi ya waokoaji yaweza kuhatarisha majeruhi kwa kuliingilia eneo la ajali mbumbumbu kama mzungu wa reli.

Hatua ya pili ni kutafuta idadi ya majeruhi. Pana uwezekano wa majeruhi kutupwa mbali na eneo la ajali. Vivyo hivyo, kuna majeruhi ambao huweweseka baada ya ajali na kuanza kutembea wasijue wanakoelekea. Wengi wao huanguka karibu na eneo la ajali au wakaenda mbali.

Hatua ya tatu ni kuchunguza kama majeruhi amezimia, moyo unapiga na jinsi anavyopumua. Ili kuhakikisha kuwa majeruhi anapumua, mwokoaji atazame kama kifua kinapanda na kushuka. Hali kadhalika, mwokoaji anaweza kusikiliza au kuguza kifua na kuona kama kuna ishara za kupumua. Iwapo majeruhi anapumua, mwokoaji amweke hali ambayo itaimarisha kupumua kwake. Anaweza akamlaza chali au kumgeuza kwa pamoja na kichwa chake ili

www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com

kufungua mkondo wa hewa. Pia anaweza kujaribu kumfanya apumue kwa kupuliza hewa mdomoni mwake. Fauka ya hayo, upulizaji wa hewa utahakikisha kuwa damu inazunguka mwilini vizuri.

Hatua nyingine ni kuchunguza vile amejehuriwa. Chunguza kama majeraha ni vidonda tu au kuna kuvunjika kwa mifupa, ni muhimu kutotumia kiungo kilichovunjika anapobebwa.

Pia, kuchunguza vile majeruhi amejehuriwa, humwezesha mwokoaji kujua huduma ya dharura atakayotumia. Majeruhi akiwa anavuja damu sana, ni muhimu kuzuia uvujaji huu. Iwapo ni kidonda kidogo, kinahitajika kufungwa ili kuzuia uambukaji. Mwokoaji anaweza kutumia kifaa chochote kilicho karibu kutolea huduma hizi. Kwa mfano anaweza kupasua nguo ya majeruhi ilia pate kitambaa cha kusaidia kuzuia kuvuja kwa damu au kumfunga kidonda.

Hatua inayofaa ni kumhamisha majeruhi kutoka eneo la ajali hadi hospitalini. Mwokoaji anaweza kuwatumia watu wengine kutafuta msaada. Wanaweza kupiga simu wakitumia nambari za simu za dharura kama zile za polisi, wazimamoto au makundi ya wataalamu wa shughuli za uokoaji. Nambari hii ya simu huwa 999 popote na haina malipo. Wanaopiga simu ni vyema kutoa maelezo ya mahali ambapo ajali imetokea, aina ya ajali na huduma za dharura zinazohitajika pamoja na idadi ya majeruhi. Iwapo makundi haya ya uokoaji yameahidi kufika, ni bora kuyasubiri.

Ikiwa makundi ya wataalamu wa uokoaji hayakupatikana, ni jukumu la mwokoaji kuhakikisha majeruhi wamehamishwa na kupelekwa hospitalini. Majeruhi wakiwa wengi ni bora kuanza na walewaliozimia au wenye matatizo ya kupua kisha kuwaendea wanaovuja damu sana. Baadaye , mwokoaji awasaidie waliovunjika mifupa huku akimalizia na wenye majeraha yasiohatarisha maisha. Ni muhimu kuwabeba majeruhi kwa kutumia machela. Hii hupunguza kuathirika Zaidi kwa majeruhi. Iwapo hamna machela karibu, mwokoaji anaweza kuunda moja kwa kutumia vipande viwili vya mbao, blanketi, shuka au makoti. Ujuzi wa huduma ya kwanza ni mojawapo ya mambo muhimu ambayo kila mtu anapaswa kuwa nayo.

visit www.freekcsepastpapers.com for more revision content

Maswali:

a) Fupisha aya mbili za kwanza kwa maneno 55-65. (alama 7, 1 utiririko)

Matayarisho.

___

___

___

Jibu.

visit www.freekcsepastpapers.com for more revision content

b) Eleza kwa kutumia maneno 90-100 hatua zinazotakiwa kufuatwa wakati wa uokoaji

(alama 8, 1 utiririko)

Matayarisho

Jibu.

visit www.freekcsepastpapers.com for more revision content

**3. MATUMIZI YA LUGHA**

A)Andika neno moja lenye sauti zifuatazo.

i) Kikwamizo sighuna cha ufizi, irabu ya mbele wastani, nazali ya midomo na irabu ya nyuma wastani.

(al 1)

………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………

ii)kipua cha ufizi, kipasuo cha ufizi, irabu ya mbele juu, nazali ya midomo, irabu ya nyuma. (al 1)

………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………..

B)i)Andika neno lenye muundo ufuatao: (al 1)

KKKI+KI

………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………

ii)Onyesha silabi katika neno (al 1)

mchuuzi

………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………

C)Weka shadda katika maneno yaliyopigiwa mstari kuleta maana iliyokusudiwa. (al 2)

Mwanafunzi akisoma <u>barabara</u> hatakuwa na <u>walakini</u> maishani.

visit www.freekcsepastpapers.com for more revision content

………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………

D)Tumia neno <u>mpaka</u> kama: (al 2)

i)nomino

………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………

ii)kihusishi

………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………..

E) Andika sentensi ifuatayo katika ukubwa wingi. (al 2)

www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com

Mlima huo ulikwewa na mwanamke yule.

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

F) i) Onyesha muundo mmoja wa ngeli ya U-I. (al 1)

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

ii) Neno halbadiri limo katika ngeli gani? (al 1)

……………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………..

G) Akifisha sentensi (al 3)

bi zuhura aliuliza Rais Uhuru atatutembelea lini

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………..

H) Unda sentensi yenye kishazi tegemezi ambacho ni kivumishi. (al 1)

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………..

I)Tunga sentensi yenye muundo ufuatao: (al 2)

KN(N+V) +KT(T+RH+RE)

visit www.freekcsepastpapers.com for more revision content

……………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

J) Changanua sentensi ifuatayo kwa jedwali. (al 3)

Ambacho kilipotea kilipatikana jana.

www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com

K) Andika kinyume cha sentensi hii. (al 2)

Wananchi wengi walihudhuria mkutano ndani ya uga wa kitaifa.

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

L)Yakinisha sentensi ifuatayo: (al 2)

Usiposoma kwa bidii hutafaulu maishani.

…………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………

M)Ainisha shamirisho katika sentensi. (al 3)

Mwajuma amemjengea nyanyake mkubwa nyumba ya msonge kwa nyasi ndefu.

…………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………………………

visit www.freekcsepastpapers.com for more revision content

N) Andika katika usemi wa taarifa. (al 2)

Karen:Tafadhali usiukanyage mguu wangu.

Chemosi:Ah!Mbona niukanyage?

…………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………………………

O) Tunga sentensi moja katika wakati uliopita hali timilifu. (al 2)

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

P) Andika upya ukianza kwa yambwa tendwa. (al 2)

Mvua iliwanyea wanunuzi sokoni hivi majuzi.

…………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………..

Q) Tunga sentensi MOJA kutofautisha maana ya fito na vito. (al 2)

…………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

R) Eleza maana mbili za sentensi: (al 2)

Dumu na mwanawe Bor ni waimbaji hodari.

…………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

S) Eleza matumizi ya **Ku** katika sentensi. (al 2)

Sikumwelewa alivyoeleza namna ya kuwatunza mbwa wake.

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

visit www.freekcsepastpapers.com for more revision content

**4 ISIMUJAMII**

**a)** Umepewa nafasi ya kutoa risala za rambirambi na heshima za mwisho katika siku ya mazishi ya rafiki yako aliyeaga dunia, eleza sifa za kimtindo utakazotumia. ***(alama 5)***

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

**b)**Fafanua changamoto tano zilizokumba maenezi ya Kiswahili nchini Kenya punde tu baada ya kupata uhuru (alama 5)

visit www.freekcsepastpapers.com for more revision content